JESMA 006

# JARIBIO LA SITA K.C.P.E
# DARASA LA NANE 2021

**KISWAHILI**
**SEHEMU YA KWANZA:**
**LUGHA**

**Muda: Saa 1 dakika 40**

## SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika KARATASI YA MAJIBU na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

## JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   NAMBA YAKO YA MTIHANI
   JINA LAKO
   JINA LA SHULE YAKO

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule. Na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

**Katika kijitabu cha maswali:**

11. Chagua jibu lenye nomino zilizo katika ngeli ya I - I pekee.
   A. kahawa, fedha;
   B. chumvi, chupa
   C. sukari, mvua
   D. mali, chai

Jibu sahihi ni C

1 [A] [B] [C] [D]    11 [A] [B] ▬ [D]    21 [A] [B] [C] [D]    31 [A] [B] [C] [D]    41 [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 11, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa**

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi ya mtihani zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

: www.jesmapublishers.com    Barua pepe: jesmapublishers@yahoo.com

© Jesma Publishers & Education Boosters Ltd.Simu: 0202217088/0701545759/0734207811

FUNGUA UKURASA

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.*

Familia ni __1__ mojawapo __2__ muhimu sana katika jamii. Mtoto hujifunza mengi kutokana na familia yake. Anapofikwa na jambo __3__, yeye hukimbilia pale __4__. Isitoshe, yeye hufunzwa ukakamavu; yaani __5__. Sifa hii __6__ kukabiliana na changamoto mbalimbali katika __7__ wake. Halikadhalika, mtoto __8__ kwa familia yake.

1. A. kituo B. asasi C. mahali D. urithi
2. A. iliyo B. walio C. kilicho D. palipo
3. A. lolote mbaya B. yoyote baya C. yoyote mbaya D. lolote baya
4. A. kulindiwa B. kuelezwa C. kuliwazwa D. kuhimizwa
5. A. hali ya kutokubali kushindwa kwa urahisi.
   B. hali ya kuvumilia shida za wengine.
   C. hali ya kutegemea msaada wa wengine.
   D. hali ya kuepuka mambo yenye madhara.
6. A. ndio unaomwandaa B. ndiyo inayomwandaa C. ndivyo inavyomwandaa D. ndio inaomwandaa
7. A. aushi B. mustakabali C. maisha D. ubunifu
8. A. hujitambulisha B. hutambua C. hutambuana D. hutambulisha

Mashaa alikuwa haambiliki __9__. Alikuwa __10__ vijana ambao __11__ kuwa kushauriwa ni kuingilia uhuru wao. __12__ angalijua kuwa __13__! Mambo yaliendelea hivi hadi siku __14__ na ya kumfika. Siku hiyo, __15__ na polisi aliponaswa akirandaranda mjini wakati wa usiku.

9. A. hasikilizi B. hasemeki C. hasemezeki D. haambiwi
10. A. kati ya B. mithili ya C. baadhi ya D. fauka ya
11. A. wangesadiki B. wamesadiki C. wakisadiki D. husadiki
12. A. Bora B. Laiti C. Aghalabu D. Angaa
13. A. uhuru jambo halisi kuukosa ni taabu.
    B. ujana tembo la nazi halikawii kutoweka.
    C. sitawaliwi hufa akitangatanga.
    D. ugwe hukatikia pembamba.
14. A. alipofikwa B. aliofikwa C. akafikwa D. alifikwa
15. A. alitiwa shemere B. alibwaga zani C. alitiwa mbaroni D. alishikwa sikio

*Kuanzia namba 16 mpaka 30, chagua jawabu lifaalo zaidi.*

16. Chagua sentensi yenye kiambishi <u>ki</u> cha ngeli pekee
   A. Mwalimu akisahihisha kitabu nitadurusu.
   B. Omari atanisalimia akielekea sokoni.
   C. Walipotuona walitembea kijeshi.
   D. Mwenda alikiokota alipokuwa ufukweni.

17. Jozi ipi ina nomino za ngeli ya <u>U-YA</u> pekee?
   A. ubua, majani
   B. mali, maafa
   C. maradhi, ubele
   D. upishi, malezi

18. Tambulisha kauli ya <u>kutendewa</u> ya sentensi ifuatayo.
   Tito alichukua kalamu ya Maria.
   A. Kalamu ya Maria ilichukuliwa na Tito.
   B. Kalamu ilichukuliwa Maria kwa Tito.
   C. Maria alichukuliwa kalamu na Tito.
   D. Maria alichukuliwa kalamu kwa Tito.

19. Fundi wa kufua visu huitwa
   A. mjume
   B. mjumu
   C. mhandisi
   D. sonara

20. Andika sentensi ifuatayo katika hali ya umoja.
   Nyembe zilizonunuliwa zitahifadhiwa mikobani mle.
   A. Wembe ulionunuliwa utahifadhiwa mkobani ule.
   B. Wembe ulionunuliwa utahifadhiwa mkobani ule.
   C. Nyembe iliyonunuliwa itahifadhiwa mkobani mle.
   D. Nyembe iliyonunuliwa itahifadhiwa mkobani ule.

21. Ni kundi lipi lenye vivumishi pekee?
   A. jeupe, kabisa, zuri, zote
   B. kabla ya, vyema, tamu, hapo
   C. dhaifu, pengine, vizuri, lile
   D. daima, nene, halafu, tele

22. Wingu ni kwa nzige kama vile ______ ni kwa mtama.
   A. kipeto
   B. tonge
   C. tano
   D. kishazi

23. Maelezo yapi ni sahihi?
   A. Bunda ni kushindwa mtihani lakini buda ni mtu asiye na meno.
   B. Bada ni jengo la muda ilhali banda ni ugali wa unga wa makopa.
   C. Ridhi ni kumiliki mali ya marehemu lakini rithi ni kukubali jambo.
   D. Vua ni kuondoa kilichovaliwa ilhali fua ni kusaidia mtu.

24. Tegua kitendawili kifuatacho.
   Saa yetu kadiri inavyofanya kazi ndivyo inavyopunguza nguvu.
   A. Moyo
   B. Mwezi
   C. Upepo
   D. Mvua

25. Andika usemi wa taarifa wa sentensi ifuatayo.
   "Nitatoa ushahidi wangu kesho", akasema.
   A. Amesema kuwa atatoa ushahidi wake kesho.
   B. Alisema kuwa atatoa ushahidi wake siku iliyofuata.
   C. Alisema kuwa angetoa ushahidi wake siku ambayo ingefuata.
   D. Alisema kuwa angetoa ushahidi wake siku ambayo inafuata.

26. Chagua methali inayotuonya dhidi ya kupuuza matatizo ya wengine.
   A. Usiwatukane wakunga na uzazi ungalipo.
   B. Fisi akila mwele mzima funga mlango.
   C. Kuvuja kwa pakacha nafuu kwa mchukuzi.
   D. Maji ya kifuu ni bahari ya chungu.

27. Tambulisha neno lenye silabi ya sauti mwambatano.
   A. Bidii
   B. Punda
   C. Mchwa
   D. Maktaba

28. Aina ya msumari wenye hesi huitwaje?
   A. Bisibisi
   B. Jiriwa
   C. Parafujo
   D. Timazi

29. Nomino gani **haiundwi** kutokana na kitenzi. **Amini**?
   A. Amani
   B. Imani
   C. Uaminifu
   D. Muumini

30. Kula mwata ni sawa na kula ________
   A. mwande
   B. njama
   C. nyara
   D. mumbi

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali kuanzia* **31** *mpaka* **40.**

Tabia nzuri na mbaya huonekana katika matendo ya binadamu. Aliye na matendo mema hustahiwa na kuthaminiwa na adinasi wengi. Lakini mwenye hulka zisizonyooka huonekana kama mahoka na watu wengi humwambaa kama shetani.

Watu katika jamii huweza kuishi kwa pamoja kwa sababu anuwai. Maingiliano haya yanahitaji kuongozwa ili wasiumizane bali waweze kuishi kwa amani na utangamano. Katika kila jamii ya kisasa, kuna sheria zinazoongoza na kudhibiti maingiliano ya watu na kuhakikisha kuwa utangamano unadumishwa. Hapa nchini Kenya, sheria hizi huundwa na bunge. Yeyote anayekiuka sheria hizo huadhibiwa na mahakama.

Kwa upande mwingine, kuna kanuni nyingine za kijamii ambazo hazikuundwa na bunge. Sheria hizi zinaitwa kaida za jamii na mwanajamii yeyote anawajibika kuzitii. Kinyume na sheria za nchi, kanuni za kijamii hazidhibitiwa na **dola** za nchi kupitia polisi na mahakama, bali mtu huweza kuzipokea kutokana na jamii anapokua.

Mojawapo ya kanuni hizi ni kuwa na huruma kwa wengine. Huruma ni kujali maslahi ya watu wengine na kuwafanyia wema. Jamii yahitaji raia kuwa na moyo wa utu, kuwapenda wengine na kuwaonea huruma. Hayo yanaweza kuonekana kupitia kuwaauni walio na mahitaji. Aidha, hudhihirika katika kuheshimu vitu vya wengine. Hatupaswi kuvichukua vitu vya wengine pasipo idhini yao.

Kanuni nyingine ni ustahimilivu. Kenya ina makundi ya waja wenye tofauti mbalimbali. Twahitaji kuonyesha stahamala kwa wote hawa katika maingiliano yetu. Kila mtu ana haki zake ambazo lazima ziheshimiwe. Lazima pia tuheshimu maoni na hadhi ya kila raia. Hatupaswi kumbagua insi yeyote kwa hali yoyote ile iwe ni kwa misingi ya kikabila, dini, rangi, elimu au mali.

Utiifu ni kanuni nyinyine. Yatupasa kutekeleza majukumu tuliyopewa kwa wakati kwani tusipofanya hivyo tutawatatiza wengine. Mathalani, tusipolinadhifisha darasa wakati wa zamu yetu tunawahasiri wengine kwani watakaa katika mazingira machafu. Yatupasa pia kutoa huduma bila kunung'unika wala kuhesabu mara tulizosaidia au gharama tulizopata.

Jamii yatuasa tuwe waaminifu kwa kupiga vita hulka kama vile ufisadi. Watu **wanaopanda, kupalilia na kunyunyizia maji mbegu ya ufisadi** ni adui wa nchi yao. Kutokana na vitendo vyao vya ufisadi, waja wengi wasio na hatia huteseka. **Wakati mwingine** taifa zima hulazimika kulipia madhara yatokanayo na **ufisadi**. Wanaoongozwa na tamaa ya utajiri, kwa mfano, hufyeka misitu yetu. Bila shaka, watu kama hawa wanatuandalia jangwa. Je, vijana tuko tayari kuishi jangwani?

Uaminifu na utiifu wahitajika katika familia. Wanajamii wote hulazimika kuonyesha uaminifu kwa asasi ya familia kwa kujiepusha na mambo yanayoweza **kuwapaka tope**. Mathalani, kijana mwaminifu kwa aila yake hawezi kushiriki katika vitendo vya fedheha kama vile mapenzi kabla ya

ndoa au kutumia afyuni. Huenda kijana huyo akapata ukimwi au mimba ambayo hakuipangia. Huyu utakuwa mzigo kwa familia yake.

Kutendeana haki ni kaida nyingine. Haki ina maana kuwa tuna wajibu wa kutenda kulingana na inavyotakikana. Yampasa mtu kujua mema na mabaya ili atende yanayofaa. Pia afahamu haki zake na za wenzake pamoja na wajibu unaoandamana na haki hizo. Yatakiwa kujua kuwa mtu anaweza kujitendea haki yeye mwenyewe na kuwatendea wenzake. Haki yadai kuwa kila wakati tukisie athari ya matendo yetu kabla ya kutenda. Ikiwa jambo litakuwa na athari mbaya kwako au kwa wengine si vyema kulifanya.

Kwa kifupi, jamii yahitaji kukuza maadili mema iwapo watu wanataka kuishi kwa amani na utangamano. La sivyo, maisha yatakuwa ya shida, dhiki na msukumano kama ya hayawani porini. Jamii ya mwenye nguvu mpishe si jamii nzuri ya mtu kuishi.

---

**31.** Chagua jibu sahihi kulingana na aya ya kwanza.
- A. Mtu huthaminiwa kutokana na tabia nzuri au mbaya.
- B. Mja hutukuzwa pale aonyeshapo mienendo iliyonyooka.
- C. Mwenye hulka zisizonyooka huitwa shetani na watu.
- D. Matendo yoyote huweza kuwafanya watu kumwambaa mja.

**32.** Umuhimu wa kuwa na sheria katika jamii ni,
- A. kuonyesha kwamba hakuna aliye juu ya sheria.
- B. kuchunguza kaida za jamii mbalimbali.
- C. kuhakikisha kuwa watu wote wanasaidiwa.
- D. kuwezesha watu kuingiliana bila kuumizana.

**33.** Kulingana na mwandishi,
- A. yapo makundi mawili ya sheria.
- B. sheria zote hutungwa na bunge.
- C. baadhi ya sheria hutungwa na mahakama.
- D. sheria za nchi si muhimu kama kaida za jamii.

**34.** Huruma ya mja hudhihirika kwa,
- A. kutaka kuhudumiwa unapokuwa na shida.
- B. kuwatambulisha wanaohitaji msaada.
- C. kuonyesha ukarimu kwa walio na mahitaji.
- D. kuwapenda wengine ili ujue shida zao.

**35.** Manufaa ya ustahimilivu kwa taifa ni kuwa,
- A. huwawezesha raia kuheshimu vitu vya wengine.
- B. hutambulisha tofauti za makundi mbalimbali.
- C. hutuwezesha kuheshimu mielekeo ya wengine.
- D. huwafanya raia kuelewa shida za wengine.

**36.** **Kupalilia na kunyunyizia maji mbegu ya ufisadi,**
- A. ni tabia ya raia wasiokuwa watiifu.
- B. ni tatizo linaloweza kuliporomosha taifa.
- C. sanasana huwa ni tabia ya viongozi.
- D. hutokea kwa nadra katika jamii zetu.

**37.** Vijana hukiuka kanuni za jamii kwa,
- A. kutelekeza majukumu yao, kuingilia nyendo potovu.
- B. kuwatatiza wenzao, kupuuzwa na familia.
- C. kutokuwa watiifu, kupata mimba za mapema.
- D. kukiuka wajibu wa wenzao, mapenzi ya kiholela.

**38.** Msemo <u>**kuwapaka tope**</u> jinsi ulivyotumika una maana ya
- A. kuwatia hasara
- B. kuwachafua roho
- C. kuvuruga uhusiano
- D. kuwaharibia sifa

**39.** Si kweli kusema kwamba,

A. kujua matokeo ya jambo ni muhimu katika kutenda haki.
B. mtu anaweza kujitendea haki yeye mwenyewe.
C. tusipowajibika tutakiuka haki zetu na za wenzetu.
D. afyuni na UKIMWI hutokana na mtu kutotendewa haki.

**40.** Neno **dola** kulingana na kifungu lina maana ya

A. sarafu ya Marekani.
B. utawala na mihimili yake.
C. kidole cha kutilia sahihi.
D. kanuni za jamii.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali kuanzia* **41 - 50.**

Kaka Mbweha, kama alivyojulikana kote, aliheshimika sana katika himaya ya wanyama. Hili lilitokana na vipawa vyake anuwai vilivyodhihirika wazi kwa wenzake. Wanyama walipokabiliwa na matatizo, Mbweha aliwatatulia na hata kuwapa ushauri bila kuwatoza malipo. Hata miradi ilipohitajika kuanzishwa katika himaya yao wanyama wangepitisha kwa kauli moja kuwa Kaka Mbweha awe mwangalizi . Mbweha naye alijitoa mhanga kuhakikisha kwamba alizitekeleza shughuli za aina hii kwa uwajibikaji mkubwa.

Jingine ambalo halikuwapita wanyama ni namna Kaka Mbweha alivyoingiliana vyema na vijana. Kila mara alipokuwa katika shuguli zake za useremala, ungewapata vijana wakipiga randa, kukereza mbao, kupiga msasa huku wengine wakitoboa mbao kwa keekee. Kama walivyosema wahenga, **mtegemea nundu haachi kunona**. Baadhi ya vijana hawa waliinukia kuwa mafundi maarufu sana katika ufundi isitoshe, vijana hawa walifaidi busara ya Mbweha kwa kupata nasaha kuhusiana na masuala yanayoathiri vijana, mathalani mapenzi kabla ya ndoa, mihadarati, shinikizo la rika na uchechefu wa nafasi za ajira.

Haieleweki vizuri ni yapi yaliyomvamia Kaka Mbweha; moyo wake ukaota gugu la inda. **Akawa joka la mdimu kuwalinda watundao**. Tangu hapo ikawa nadra sana kumpata katika karakana yake. Hata alipofika, alidai kwamba shughuli za siku zilikuwa kidogo tu; hakuhitaji msaidizi. Vijana wakalazimika kuondoka pale shingo upande. Badala ya zile lulu alizowapakulia kila uchao, sasa akaanza kuwa mnyamavu. Ambacho wanyama hawakujua ni kwamba Kaka Mbweha alibadilika hivi ili wanyama wautambue umuhimu wake.

Wakati mmoja, mtoto wa Ndovu alishikwa na maradhi ambayo yalimtaabisha sana. Kwa majuma kadhaa, hata wazazi wake hawakutoka maadamu walimwuguza mwana wao mchana kutwa na usiku kucha. Hata wanyama wengine wakajipata wakija kwa zamu kuiliwaza jamaa hii ni kuto msaada palipohitajika. Mbweha pekee ndiye hakufika. Hali hii ilishangaza. Yeye alijulikana kw tajiriba yake pana ya kutibu maradhi yaliyowatoa jasho hata waganga na waganguzi. Vipi mara h akauficha mchango wake uliohitajika sana?

Wanyama walifanya kikao cha dharura. Baada ya kushauriana, walikata shauri kumtu mmoja wao akamfuate Kaka Mbweha. Nyani alijitolea kwa shughuli hiyo. Alipofika, alimku Mbweha nje ya kibanda chake akicheza na mwanawe. Salamu za Nyani zilijibiwa kwa sau baridibaridi. Ingawa akufukuzaye hakwambii toka, Nyani alielewa kuwa uso wa kufadhiliwa chini. Basi kwa unyenyekevu mkubwa, akaeleza haja yake ya kuwa pale. "Nenda uwajulishe ku nikipata wakati nitakuja", Mbweha akajibu kisha Nyani akaondoka.

Nyumbani kwa Ndovu, wanyama walisubiri huku hali ya mtoto ikizidi kuzorota. Hatima waliposubiri kiasi cha kukata tamaa, Mbweha alionekana kwa mbali akija. Alipofika, wanya walijitenga kumpa nafasi. Alimpa mtoto yule dawa na baada ya muda mfupi, mtoto akaanza kup afueni. Wanyama walifurahi na kushangilia sana. Kisha. Mbweha aliwapa wazazi dawa, akawael masharti ya kuzingatiwa kisha akajiandaa kutoka.

"Ngoja kidogo", akasema Nyani," vipi unaondoka bila shukurani zetu?" Kaka Mbweha na wanyama wengine walipotulia, Nyani alimsifu Mbweha kwa mengi aliyoifanyia jamii ya wanyama. Alimpa shukrani za dhati kutoka kwa kinara wao simba. Wakati huo, mtima wa Mbweha ulikuwa ukidunda kwa fahari kuu. "Sasa wamejua thamani yangu," Mbweha akajisemea kimoyomoyo. "Watanitafuta hata zaidi. Sitakuwa mwepesi wa kupatikana"

Hata hivyo, maneno yaliyofuatia ndiyo yaliyomchoma Mbweha ipasavyo. Shukrani za Nyani hazikukomea hapo. Aliwashukuru Ndovu na Kifaru kwa kujitolea kuihami jamii kutwa kucha. Akatambua jitihada za ng'ombe kuwapa wanyama wote maziwa pasipo kulalamika,kurumbiza na ninga kwa kuwatumbuiza walipofanya kazi....... orodha ilikuwa ndefu. Mbweha akatanabahi kwamba wapo wengine waliotoa hata mchango mkubwa zaidi yake pasipo kujionyesha. Alijikuta kainamisha uso asijue la kufanya.

Hotuba ya Nyani ilipofikia tamati; Mbweha alikichukua kipazasauti. Kwa unyenyekevu. aliwaomba wenzake msamaha na kuahidi kuunga mkono jitihada zote za kuisimamisha jamii ya wanyama.

41. Ni kweli kuwa Kaka Mbweha,
   A. alikuwa kiongozi katika himaya ya wanyama.
   B. alikuwa mwepesi wa kutatua mambo mbalimbali.
   C. alitunukiwa vipawa kuliko wanyama wote.
   D. alijulikana na kupendwa na hata wasiomjua.

42. Wanyama walimteua Mbweha kusimamia miradi yao, kwa sababu ya
   A. umaarufu wake.
   B. uangalifu wake.
   C. unyenyekevu wake.
   D. maarifa yake.

43. Methali '**Mtegemea nundu haachi kunona**'imetumika kuonyesha kwamba,
   A. vijana walimwandama Mbweha ili kufaidi maarifa yake.
   B. Mbweha aliwatumikisha vijana ili kujiongezea kipato.
   C. karakana ya Mbweha ilifaidika kwa mchango wa vijana.
   D. Vijana wenye maarifa waliunda samani za thamani.

44. Chagua sifa za Kaka Mbweha kwa mujibu wa makala haya.
   A. Mwenye majisifu, asiyejali hisia za wengine.
   B. Mkaidi, mwepesi wa kukasirika.
   C. Mkono wazi, anayetaka kutambuliwa.
   D. Mchoyo, anayewabagua vijana.

45. Lipi **SI** kati ya matatizo yanayowakabili vijana katika jamii ya wanyama?
   A. Ndoa za mapema.
   B. Maradhi ya zinaa.
   C. Matumizi mabay[illegible] ya dawa.
   D. Ukosefu wa kazi

46. Kulingana na aya ya [illegible]ne.
   A. Magonjwa yalikw[illegible]misha shughuli zote katika himaya ya wanyama.
   B. Wanyama walithaminiana na kujaliana maslahi.
   C. Wanyama wote walifika kuipoza familia ya Ndovu.
   D. Wengi hawaamini kuwa Mbweha angeweza kumtib[illegible] mtoto.

47. "Nenda uwajulishe kuwa nikipata nafasi nitakuja". Maneno haya yanaonyesha kwamba,

A. Mbweha amekataa kuenda kwa Ndovu.
B. Mbweha amekabiliwa na shughuli nyingi.
C. Mbweha ameingiwa na kiburi.
D. Mbweha amekereka kwa kumwona Nyani.

48. Pindi tu mtoto alipopewa dawa,

A. hali yake ilianza kuimarika.
B. alipona na kuanza kufanya shughuli zake.
C. Mbweha alifunganya virago akaondoka.
D. Wanyama walishangilia kwa furaha.

49. Kauli 'Akawa joka la mdimu kuwalinda watundao" imetumia tamathali gani ya usemi?

A. Chuku
B. Tashbihi
C. Jazanda
D. Sitiari

50. Funzo linalotokana na kifungu hiki ni kuwa,

A. Wale wenye vipawa ndio waingiwao na kiburi.
B. Kupuuza juhudi za wengine ni njia ya kuwavunja moyo.
C. Mola ametutunuku vipawa mbalimbali ili kuzifaidi jamii zetu.
D. Mchango wa wengine ni muhimu kuliko ule tutoao.